**102/3**

**KISWAHILI**

**KARATASI YA 3**

**FASIHI**

**JUNI/JULAI 2022**

**MUDA: SAA 2½**

# MTIHANI WA MWIGO, ENEO-BUNGE LA

# MUMIAS MAGHARIBI

## Cheti cha Kuhitimu Masomo ya Sekondari Kenya (K.C.S.E)

**MAAGIZO**

a) Jibu maswali **manne** pekee.

b) Swali la **kwanza** ni la **lazima.**

c) Maswali hayo mengine **matatu** yachaguliwe kutoka **sehemu nne** zilizobaki yaani, **Riwaya, Tamthilia, Ushairi** na **Hadithi Fupi.**

d) Usijibu maswali **mawili** kutoka sehemu moja.

e) Majibu yote lazima yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili.

f) Kila swali lina alama **20**.

g) Karatasi hii ina kurasa **8**. Watahiniwa ni lazima waangalie kama kurasa zote za karatasi hii zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo.

# SEHEMU A: FASIHI SIMULIZI (LAZIMA)

Soma kifungu hiki kisha ujibu maswali.

Umeanguka mwamba
Jabali tuloegemea
Lilotupa kimbilio
Mahasidi kutishia
Mti mkuu umegwa
Wana wa ndege wa wapi?
Bila shaka hangaiko
Metukumba makinda.

Angalikuwa pamwe nasi
Maulana mungu wetu
Swali hilo tungemuuliza
Mbona kaacha mauko
Ngome yetu kuvamia?
Ela mwenyewe Mwenza
Ajua hatima yetu
Lilobaki kumwamini
Riziki kutuangushia.

Maswali

a. Huu ni wimbo wa aina gani? Thibitisha. Alama 4
b. Bainisha vipengele vitano vya kimtindo vilivyotumika katika wimbo huu. Alama 5
c. Tungo za aina hii zinaendelea kupoteza umaarufu katika jamii yako. Fafanua hoja nne utakazotumia kuishawishi jamii yako kukinga dhidi ya hali hii. Alama 4

d. Eleza sababu tatu za kukusanya habari kuhusu kipera hiki kwa kutumia mbinu ya kushiriki. Alama 3
e. Ainisha kifungu kifuatacho cha sifo. Thibitisha kwa hoja tatu. Alama 4

Ndimi Kiluki jogoo la kijijini
Jogoo la kijijini liwikialo jijini
Jogoo liloyavunja makoo ya jijini
Makoo yote yanisifia
Wangu ukoo ni wa wafalme
Kilimo ndo nguzo yetu
Kiluki nalima maekari kwa maekari
Siku chache natumia
Kandanda nasakata
Asonijua Makinduni ni nani?
Mbeleni ajitambulishe.

## SEHEMU B: RIWAYA

## ASSUMPTA K. MATEI: CHOZI LA HERI

## Jibu swali la 2 au 3

2. "Sikiliza bwana, mhitaji siku zote ni mtumwa, tangu lini maskini akabagua?

   a. Weka dondoo hili katika muktadha wake. Alama 4
   b. Eleza namna anayeambiwa maneno haya alivyoendeleza ploti ya riwaya ya Chozi la Heri. Alama 6
   c. Kwa mujibu wa riwaya hii, maneno ya msemaji ni ya kweli. Thibitisha kwa hoja kumi. Alama 10.

3. a. Changanua mtindo katika dondoo hili: alama 12

Sisi tunataka kiongozi yeyote awe mwanamke au mwanamme, atakayeweza kulielekeza jahazi hili letu kwenye visiwa vya hazina. Tufikie kilele cha maendeleo pale tutakapoafikia malengo ya Kimaendeleo ya Kimilenia. Kiongozi ambaye ataendeleza zaidi juhudi za kukabiliana na wale maadui ambao wewe daima huniambia kuhusu: umaskini, ujinga, magonjwa, uhaba wa nafasi ya kazi na ufisadi. Je, huu sio uliokuwa muono wa waliopigania uhuru? Siyo ambayo viongozi waliochukua hatamu za uongozi kutoka kwa watu weupe waliyofanya juu chini kuyatekeleza?

b. Mwalimu amekwezwa katika riwaya ya Chozi la Heri. Thibitisha. Alama 8.

## SEHEMU C: TAMTHILIA

## PAULINE KEA: KIGOGO

## Jibu swali la 4 au 5

4. a. Mhini na mhiniwa njia yao ni moja. Thibitisha ukweli wa kauli hii kwa mujibu wa tamthilia ya kigogo. Alama 10

b. Fafanua vizingiti mbalimbali vinavyojitokeza katika harakati za Wanasagamoyo kuikomboa jamii yao. Alama 10

5. Sina muda wa kupoteza tafakuri zangu kwa mambo yasiyoniruzuku…safari hii ni hatua kwa hatua.

a. Weka dondoo hili katika muktadha wake. Alama 5

b. Bainisha toni iliyotumika katika kauli hii. Alama 2

c. Eleza umuhimu wa mandhari ambamo kauli hii inajitokeza. Alama 8

d. Jadili sifa zozote tano za msemaji wa maneno haya. Alama 5

## SEHEMU D: USHAIRI

## Jibu swali la 6 au 7

6. Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.

**Wanaume ni wanyama**

Nakumbuka vyema sana, sisahau siku ile
Nilipoitwa na nina, akanipa ya kivyele
Mwanangu u msichana, nakuasa usikile
Si watu waone vile, wanaume ni wanyama.

Kuwa umevunja ungo, ni hali ya maumbile
Bora uwapo na bongo, anasa uzikimbile
Ukijitia maringo, utatungwa mimba mbele
Si watu waone vile, wanaume ni wanyama.

Ngawa waje na manoti, “Nakupenda” wakwambile
Wakuvalie makoti, usiwaachie mbele,
Hata wapige magoti, wambile mna kelele
Si watu waone vile, wanaume ni wanyama.

Ngono ni tendo la suna, Amina sikimbilile
Wala miguu halina, kwamba lingekukimbile
Muhimu kwako Amina, kwanza uthamini shule
Si watu waone vile, wanaume ni wanyama.

Kuzurura mitaani, si tabia njema ile
Unapotoka nyumbani, fululiza hadi shule
Si kwenda vichochoroni, kuwaona kina wale
Si watu waone vile, wanaume ni wanyama.

Uwe mwana msikizi, yano uyazingatile
Mengine kuhusu penzi, mwanangu taonywa shule
Kama mameyo mzazi, nimekuonya kimbele
Si watu waone vile, wanaume ni wanyama.

Wakaja kina Hamadi, mwana wa Mzee sule
Kwangu wakapiga hodi, hata mkuu wa shule
Ila nikajitahidi, kukwepa mitego ile
Si watu waone vile, wanaume ni wanyama.

Na kuna huyo Karisa, mwanafunzi kule shule
Akawa hunipapasa, nami vile vile
Mwishowe ikatupasa, tugawe tunda tule
Si watu waone vile, wanaume ni wanyama.

Nani akachovya uto, wa asali tamu vile
Na kisha aape kuto, kula asali milele
Kuwa ni mjamzito, wamenifukuza shule
Si watu waone vile, wanaume ni wanyama.

Karisa yu vilevile, angali yuwaenda shule
Na mie kitumbo mbele, ninajikuna upele
Yameshatimia yale, niloonywa siku ile
Si watu waone vile, wanaume ni wanyama.

**Maswali**

a) Eleza ujumbe wa shairi hili? alama 5

b) Ainisha shairi hili kwa kuzingatia vigezo vifuatavyo: alama 3

i. vina

ii. vipande

iii. mishororo

c) Onyesha umuhimu wa mbinu mbili alizotumia mshairi kutosheleza mahitaji ya kiarudhi katika shairi hili. alama 2

d) Tambua nafsi neni katika shairi. Thibitisha alama 1

e) Andika ubeti wa sita kwa lugha nathari. alama 4

f) Tambua aina mbili za urudiaji zilizotumika katika shairi hili. Alama 2

g) Eleza maana za maneno na vifungu vya maneno vifuatavyo: alama 2

i. anasa uzikimbile

ii. wanaume ni wanyama

iii. tugawe tunda tule

7. Soma shairi hili kisha ujibu maswali.

Nikumbuke mwanangu,
Kila asubuhi unapoamka,
Kwenda kazini,
Unapochukua sabuni ya kunukia,
Na dodoki jororo

Na kopo la koligeti,
Kwenda kukoga hamamuni,
Penye maji ya bomba,
Yaliyochunjwa na kutakaswa,
Mororo…

Kumbuka nyakati zile,
Za staftahi ya sima na mtama,
Ndizi na nagwa,
Kwa mchicha na kisamvu,
Na ulipokwenda choo,
Ulilia kwa uchungu,

Nikumbuke,
Unapotoka nyumbani asubuhi maridadi,
Katika suti ya moto,
Miwani ya pembe,
Viatu vya Paris,
Saa ya dhahabu,
Unapong'oka kwenda kazini,
Katika Volvo,
Katika njia iliyosakafiwa.

Kumbuka,
Nyakati zile,
Mimi ni mamako,
Tulivyojidamka,
Mara tu kwale wa kwanza,
Alipoanza kukoroma,

Jogoo wa kwanza hajawika,
Mimi nikachukua mundu na panga,
Mamako jembe na shoka,
Tukaelekea porini,
Kufyeka na kuchimbua,
Na hubaki wajiandaa kwenda shule..
Nikumbuke,
Saa za jioni,
Unapovalia kitanashati

**Maswali**

a) Thibitisha kuwa utungo huu ni shairi (alama 4)
b) Fafanua toni ya utungo huu (alama 2)
c) Huku ukitoa mifano, linganua kati ya mistari toshelezi na mistari mishata (alama 4)
d) Eleza maudhui yoyote manne yanayojitokeza (alama 4)
e) Tambua aina mbili za taswira zilizo katika ubeti wa mwisho. (alama 2)
f) Eleza muundo wa shairi hili. (Alama 4)

## SEHEMU E: HADITHI FUPI

## Wah. Alifa Chokocho na Dumu Kayanda: TUMBO LISILOSHIBA NA HADITHI NYINGINE

## Swali la 8

8a. Eleza umuhimu wa mazungumzo kati ya Sasa na Mbura katika kujenga hadithi ya Shibe inatumaliza. Alama 10

b. Fafanua jinsi suala la malezi lilivyoshughulikiwa katika hadithi ya Tulipokutana Tena na Mtihani wa Maisha. Alama 10

HUU NI UKURASA WA MWISHO.